

CultureTalk Tanzania Video Transcripts: <http://langmedia.fivecolleges.edu>
Beaches and Bagamoyo

Swahili transcript:

Upendo: OK. Sasa tuzungumzie kuhusu sehemu za viburudisho labda niseme *recreational centers* katika Tanzania. Labda tuanze na wewe. Umeshawahi kwenda sehemu yoyote katika kwenda kujiburudisha labda baada ya kazi ngumu, nzito, nini. Au labda ulipokuwa ukisoma shule, umeshawahi kwenda sehemu zozote za kuweza ku...?

Happy: Kujiburudisha?

Upendo: Mmmh!

Happy: Aaah! Sehemu za kujiburudisha ziko nyingi sana. Kwa mfano, kuna sehemu za ufukweni kandokando mwa bahari, kwa mfano Msasani *beach club*.

Upendo: Mmmh!

Happy: Kule kuna upepo mzuri unavuma yaani jioni, halafu kuna bendi zinakuwa zinapiga pembeni. Ulishawahi kusikia Akudo *sound*?

Upendo: Mmmh!

Happy: Kwa hiyo hizo bendi ndio zinakuwa zinapiga. Kwa mfano Akudo sound yenyewe inapiga pale kila jumapili. Kwa hiyo kila jumapili unaweza ukaenda, ukapunga zako upepo, ukala, pia muziki huku unapigwa, kila mtu anaangalia tu bure. Kwa hiyo, hizo ni sehemu...hiyo ni sehemu mojawapo ya kiburudisho.

Upendo: Na sehemu nyingine labda ambazo wewe umewahi kwenda labda?

Happy: Kwa mfano, kuna sehemu zingine kama mfano labda Bagamoyo, ambayo pia ni sehemu ya utalii, lakini pia ni sehemu ya kiburudisho. Unaweza ukaenda. Kuna ufukwe...kuna...kuna..nini tuseme...kuna beach nyingi ambazo ziko kule ambazo watu wanaenda jumamosi kwa mfano labda familia zao. Kuna michezo ya watoto, kuna sehemu za kihistoria ambazo unaweza ukaenda ukaangalia. Mfano, magofu mbalimbali ya watu wa zamani, sehemu za utumwa. Pia kuna sehemu ambazo...yaani inaweza kuwa pia ni kima...yaani Bagamoyo ni sehemu ambayo ni kimafunzo; na pia ni sehemu ambayo ni ya kujiburudisha. Mkakaa, mka...mkapata chakula, mka-enjoy; lakini pia unaweza pia ukaenda sehemu za kama hizo za kihistoria na kujifunza mambo mengi. Kwa hiyo yaani, sanasana ni historia ya utumwa katika Afrika Mashariki; jinsi gani watumwa walikuwa wanachukuliwa, walivyokuwa wanawekwa. Sehemu za makaburi ya masultani. Kwa hiyo, hivi ni vitu ambavyo vipo kule Bagamoyo; kwa hiyo ukienda yaani..

Upendo: Ni sehemu nzuri sana ya kuweza kujifundisha. Pia kuna labda hotels labda nzuri?

Happy: Eeeh! Bagamoyo kuna hoteli nyingi!

Upendo: Ahaa!

Happy: Eeeh! Kuna hoteli kama Paradise Holiday Resort, kuna hoteli nyingine kama..aah! nimesahau majina yake, lakini yaani ziko nyingi na ni nzuri, na kila hotel iko unique. Yaani hoteli, kwa mfano ukienda Paradise, na ukaenda..aaah! nimekumbuka, nyingine inaitwa Millenium Resort; ukienda Millenium, yaani zote zipo Bagamoyo; lakini set up na kila kitu na nini tofauti. Yaani *so beautiful!*

Upendo: OK. Na mimi pia nimeshawahi kwenda sehemu hizi za viburudisho. Wakati bado tuko Dar es salaam, tulikuwa tunapenda kwenda hii beach ya huku aah!huku Coco beach.

Happy: Oysterbay.

Upendo: Mmmh! Oysterbay, tulikuwa tunaenda hii beach ya Oysterbay, Coco beach. Ukiona yale maji, bahari na nini, mchanga mweupe, yaani ni sehemu nzuri kwa kweli. Kwa hiyo kipindi hicho nimechumbiwa na Sixfrid, tulikuwa tunaenda siku za jumamosi, au jumapili. Tuna, basi tunakaa tunakula chakula chetu, tunakunywa vinywaji, tunaburudika, basi tunafurahi, tunaongea mipango yetu ya baadae, nini. Kwa hiyo, nilikuwa nafurahia sana kwa kweli, ni sehemu nzuri.

Happy: Halafu unakumbuka mihogo ya kule beach?wanakuwa wanapitisha? Ina pilipili!

Upendo: Eeeh! Mizuri, aah! ni mizuri, ni mizuri sana, unakula yaani mpaka unafurahia. Ni sehemu nzuri sana kwa kweli kwa jiji la Dar es salaam. Na mara nyingi hata wakati wa sherehe mbalimbali, utakuta watoto wanaenda mchana kule Coco beach.

Happy: Kwa mfano siku za Idd.

Upendo: Siku za krismasi.

Happy: Ila pia ni hatari kwa watoto, unajua watoto huwa wanazama. Nimeshawahi kusikia kesi nyingi watoto wanakuwa wanazama wanapokuwa wanaogelea. Watoto wanakuwa wengi, yaani inakuwa iko very crowded, lakini yaani ni nzuri.

Upendo: Yaah! ni sehemu nzuri lakini kwa watoto sasa inabidi wazazi.

Happy: Wawe makini.

Upendo: Wawe makini kuwaangalia watoto wao. Ni sehemu nzuri ambayo watoto wanaenda, wanaburudika, wanacheza, wanafurahi, wanaogelea. Sema unakuta watoto wengine ni watundu. Watoto wanaogelea sehemu.maana watoto hawapaswi kwenda mbali sana kwenye...katika bahari, kuna sehemu zingine una kina kirefu. Kwa hio utakuta mtoto mwingine kuwaonyesha watoto wenzake kwamba

Happy: Anajua sana

Upendo: Anajua kuogelea nini, sasa anaogelea anaenda mpaka ile sehemu ambayo ni kina kirefu, na unakuja kushangaa tayari keshachukuliwa na maji.

Happy: Yaah!

Upendo: Kwa hiyo, sanasana ni wazazi.

Happy: Kuwa makini.

Upendo: Yaah! kuwa makini wanapowapeleka watoto wao kule beach kwenda kuogelea na kucheza wawe makini na waweze kuwaambia labda mapema labda msiogelee mbali zaidi kwenda kwenye kina kirefu.

Happy: Mmmh!

English translation:

Upendo: Let's talk about recreational places in Tanzania. Starting with you, have you been to recreational places when you were a student?

Happy: There are many recreational places in Tanzania. For example, along the shore, there is the Msasani beach club. When you visit the Msasani beach club, you will find some live bands with the Acudo sound. It is a good place to stay, due to the good wind blowing from the Indian Ocean. The Acudo sound bands entertain at Msasani beach club every Sunday. People go there to enjoy the weather, eat, and watch live bands. And it is free. Everyone can watch these bands for free.

Upendo: Are there other places you have visited?

Happy: Another recreational and tourist place is Bagamoyo. Many people love to visit there on Saturdays with their families. There are some beaches and children's games that children can enjoy. Also, Bagamoyo is a historical place where you will find historical ruins reminding you of the colonial era. Bagamoyo is also a place where you can go and learn different things, including the slave trade in East Africa during the colonial era. You can learn how the slaves were taken, and where they were put. There are also Arab sultanate graves there. These are the things you can learn and enjoy when visiting Bagamoyo.

Upendo: It is a good place to visit. Are there good hotels in Bagamoyo?

Happy: There are many hotels in Bagamoyo

Upendo: Aah!

Happy: Yeah! There is the Paradise Hotel, Millennium Hotel and many more. I don't remember their names. And each hotel is unique -- so beautiful.

Upendo: In Dar es Salaam, I used to go to such recreational places as Coco beach.

Happy: Oyster Bay?

Upendo: Yeah, Oyster Bay beach. Being at the beach and viewing the Indian Ocean with its white sand was nice. When I was engaged to Sixfrid (who is now my husband), we used to go there on Saturdays or Sundays. We enjoyed eating, drinking cold drinks and talking about our future plans. I enjoyed it so much. It is a good place for entertainment.

Happy: Do you remember the fried cassavas they sell at Coco beach? They are so delicious.

Upendo: Yeah! The cassavas are so delicious. You will never regret eating fried cassava at Coco beach, so delicious! Dar es Salaam city is a good place for entertainment. During holidays, many children love to play and swim at Coco beach.

Happy: They go there during *Eid*.

Upendo: And Christmas.

Happy: During holidays, the beach is so crowded. Many people go there. It is dangerous for children when they play alone without attention from their parents. Some may drown in the ocean.

Upendo: Parents should be careful when they send their children to the beach to swim. They should make sure their children swim in a recommended area. But you may find other children trying to swim in a deep area. That is dangerous, as they may drown in the ocean.

Happy: Yeah!

Upendo: So parents....

Happy: Should take care of their children...

Upendo: When they send their children to the beach to play and swim, they should tell them in advance that they are not supposed to swim in deep water, or they will drown and die.

Happy: Mmm! (yeah).

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated